Al-Islam.org
Ahlul Bayt Digital Islamic Library Project
Published on *Al-Islam.org* (https://www.al-islam.org)

Utangulizi Kuelewa Ubora Wa Du'a

Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) amenukuliwa akisema:

مَنْ دَعَا بِهَذَا الدُّعآءِ فِي شَهْرِ رَمَضَان بَعْدَ الْمَكْتُوْبَةِ اسْتَغْفِرَتْ ذُنُوْبُهُ إِلى

يَوْمِ الْقِيَامَةِ

"Yeyote yule atakayeomba kwa du'a hii katika mwezi Mtukufu wa Ramadhani baada ya salat ya wajib, dhambi zake zitasamehewa mpaka Siku ya Hukumu."1

Du'a sio maneno ya mdomoni tu, bali ni hali halisi ya kuhitaji, ambayo sana inadhihirishwa na maombi ya mdomo. Maadamu hakuna upatanifu kati ya hali ya ndani ya kuhitaji, na "maneno ya mdomoni" maombi yatakosa kiini chake.

Kwa kutambua haya, tunasema kwamba "hali ya kutamani sana kwa ajili ya hali bora ya kila jamii ya wanadamu" ni "haja ya asili" ya kila mwanadamu
ambaye anafaidi roho isiyo na waa. Hii ni kwa sababu kila mwanadamu amepambiwa na sifa za Allah (s.w.t.). Na moja ya sifa hizo ni 'Rehema' (Huruma) ambayo imevienea vyote. Kwa hiyo mwanadamu kwa asili hupenda ufanisi wa kila mwanadamu mwingine. Sababu ambayo wengi wetu hatuna sifa hii, ni utenganisho wetu kutoka ukuruba wa Allah Muumba wetu Mpendwa. Kwa hiyo tunahitaji kufanya utakaso wa nafsi ili kuelewa sifa hii ambayo imefichwa kwa ajili ya wingi wa dhambi na mfungamano wa mambo ya dunia.

Na wakati tunapokuwa katika hali ya kutamani ufanisi wa wengine na kutafsiri hayo katika muundo wa maneno, maombi yetu yatabeba maana, na tutafaidika kutokana na ubora wake mkubwa. Hata hivyo, wale ambao hawakupata daraja hii ya ukuruba, hawapaswi kukata tamaa bali wasome du'a hii mara kwa mara pamoja na kutafakari. Kama du'a hii ya nuru ilikuwa imekusudiwa kwa ajili ya wanadamu wakamilifu tu, Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) asingeifundisha kwa watu wote. Kwa hiyo, wakati wote lazima

tujaribu kusoma du'a hii kwa mazingatio na kubadilika. Kama mtu angelikazia fikra za hali ya juu zilizomo kwenye du'a hii, kwa hakika anaweza kuamka kutoka kwenye usingizi wake mzito na kubadilisha maisha yake.

Katika Mwezi huu wa Baraka wakati ambapo Baraka za Allah (s.w.t.) zinamiminika bila kikomo, tumuombe Allah kwa unyenyekevu ili atuwezeshe kuwa miongoni mwa wale ambao wanasoma dua hii ya ajabu kama tafsiri ya nia zetu za ndani.

1. 'Allāma Majliisi, Bihār al- Anwār, J. 95, uk . 120 sura ya 6.

Source URL: https://www.al-islam.org/fr/node/39626#comment-0